**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**MAY, 2026**

**RUANGWA-LINDI**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**


**Namba za Simu:**

**Mkuu wa Shule: 07824414486/0782260513**

**Makamu Mkuu wa Shule-Utawala:0768513559**

**Makamu Mkuu wa shule-Taaluma:0746329429**

**Matron: 0746329429**

**Patron: 0717934535**

**Shule ya Secondary: KITANDI**

**S.L.P:36 RUANGWA.**

**............................**


**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….......................**
**S.L.P ……………………………….............**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KITANDI HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA MKOA LINDI MWAKA ...................**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka : **...............** na atasoma tahasusi ya HGL (History, Geography na English Language)

Shule ya Sekondari **KITANDI** ipo umbali wa Kilometa **05** kutoka standi kuu ya mabasi ya Mji wa **Ruangwa.** Shule ipo kijiji cha Kitandi, kata ya Likunja na ipo umbali wa mita 500 (nusu kilometa) tuu kutoka kibao cha shule kilichopo barabara kuu ya Dar-es salaam – Ruangwa.
Usafiri wa basi kutoka Ruangwa mjini: Mji wa **Ruangwa** unapatikana katika kituo cha mabasi cha **Ruangwa stendi**. Kwa wanaotokea Dar-es Salaam, Masasi au Mtwara washuke standi kuu ya mabasi Ruangwa mjini. Kutoka standi kuu nauli ya bodaboda hadi shuleni ni Tshs 4,000/ tuu.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **..................**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe : **..................** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **.....................**

**1. Mambo muhimu ya kuzingatia: -**

**1.1 Sare za Shule WAVULANA**

i. Sare ya shule hii ni (**Dark blue (bluu giza**), **suruali mbili (02)** .
Maelezo ya mshono **urefu unao gusa kiatu na upana wa heshima** (*Suruali unaweza shonea shuleni kwa Tshs 28,000/ kwa moja) kwa atakayehitaji*

ii. Mashati ya light blue (**bluu bahari) mawili (02) ya mikono mirefu na yenye kola shingoni**;

iii. Sare ya Michezo ni JEZI YA TAIFA STARS (**bukta na jezi pea moja) rangi ya blue** na **tracksuit dark blue moja(01)** na **viatu vya michezo (njumu kwa ajili ya mpira na raba kwa ajili ya jogging)**.

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

v. Soksi jozi mbili nyeusi za shule;

vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

vii. Sweta **rangi dark blue lenye kola ya ”V” moja (01)** (Inapatikana shuleni kwa Tshs 20,000/= kwa atakayehitaji

viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) **suruali mbili (02) nyeusi** na **fulana rangi ya blue** yenye nembo ya shule **mbili (02)** (Fulana zina patikana shuleni kwa Tshs 15,000/ kwa fulana moja ***kwa atakayehitaji***

ix. Tisheti (T-shirt aina form six) :**Rangi ya kijivu (gray) za darasani yenye nembo ya shule mbili (02)** (*Zina patikana shuleni kila moja Tshs 15,000/)*

**1.2 Sare za Shule WASICHANA**

x. Sare ya shule hii ni (**Dark blue (bluu giza**), **sketi mbili (02)**.
Maelezo ya mshono: **urefu unao fikia juu kidogo ya kifundo cha mguu; mtindo wa rinda box mbele na nyuma** (*sketi unaweza shonea shuleni kwa Tshs 27,000/ kila moja kwa atakayehitaji*

xi. Mashati ya light blue (**bluu bahari) mawili (02) ya mikono mirefu na yenye kola shingoni**.

xii. Kwa wanao vaa hijabu iwe ya rangi ya light blue (bluu bahari) na kitambaa aina ya haluwa na sio mpira.

xiii. Sare ya Michezo ni JEZI YA TAIFA STARS (**bukta na jezi pea moja) rangi ya blue/nyeusi; skin tight ndefu nyeusi (**yakuvalia ndani ya bukta ya michezo**)** na **tracksuit dark blue moja(01)** na **raba za michezo.**

xiv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

xv. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;

xvi. Sweta **rangi dark blue lenye kola ya ”V” moja (01)** (Inapatikana shuleni kwa Tshs **20,000/= kwa atakayehitaji**

xvii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) **sketi za rinda box mbele na nyuma mbili (02) nyeusi** (zipo shuleni kwa Tshs 27,000/ kila moja) na fulana

**rangi ya blue yenye nembo ya shule mbili (02)** (Fulana zina patikana shuleni kwa ***Tshs 15,000/*** kwa fulana moja ***kwa atakayehitaji***

xviii. **Tisheti (**T-shirt aina ya form six): **Rangi ya kijivu** (Gray) **za darasani** zenye nembo ya shule mbili (02) (Zinapatikana shuleni kila moja Tshs **15,000/)** kwa atakayehitaji

**1.3 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo:-**

i. Madaftari **Countebook quire 4 (09)** ;
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatishwa*);
iv. Scientific Calculator;
v. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
vi. Faili folder la kaki 1 na plastic 1
vii. Sanduku imara la chuma (trunker) na kufuli
viii. Godoro la sponji moja 2½, x 6''
ix. Shuka mbili (2) za rangi ya **blue** ( kwa WAVULANA) na za **pinki** (kwa WASICHANA) blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (blue)
x. Nguo za ndani za kutosha;
xi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
xii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xiii. Dawa ya chooni lita tano.
xiv. Mifangio 2, (laini 1na mgumu 1 ya dukani)
xv. Kwanja 1,squizer, mopa,sabuni ya maji (lita 5), Aro moja (dawa ya kusafishia sinki), jembe 1 na mpini wake, reki 1, .

**1.4 Michango mbalimbali**

Mzazi/mlezi utachangia michango ifuatayo kupitia akaunti Na. **0150711066700**
jina la akaunti : **KITANDI SECONDARY SCHOOL -CRDB**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| **Jumla** | | **80,000/=** |

**NB: Kwa mwanafunzi asiye na bima ya afya atatakiwa kuchangia fedha ya bima ya afya Tsh 50,400/= kwa mwaka.**

**2. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali/dawa bila idhini
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga nywele ndefu au kunyoa kipara (zungu). Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu; kwa wavulana
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi/redio katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Jina la Mkuu wa Shule : DAVID PATSON MWAKALOBO**

**Saini ya Mkuu wa Shule:**




**Muhuri wa Mkuu wa Shule :**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0782441448/0782260513**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0768513559**
- **Makamu mkuu wa shule Taaluma : 0746329429**
- **Mwandamizi Malezi : 0717934535**

# RUANGWA DISTRICT COUNCIL
# REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**THE HEADMISTRESS,**
**KITANDI SECONDARY SCHOOL,**
**P O. BOX 36,**
**RUANGWA.**
**DATE……………………………….**

**TO:**
**The Medical officer**
**………………………………………**
**………………………………………..**
**………………………………………..**
**Re: NAME………………………………………………………………………………**

Please examine the above as to his/her physical and mental fitness for full time course of Secondary education at Kitandi Secondary School.

1. Eye sight…………………………………………………………………………..
2. Hearing……………………………………………………………………………
3. Speech………………………………………………………………………………
4. Venereal diseases…………………………………………………………….
5. Neurosis……………………………………………………………………………
6. TB……………………………………………………………………………………

Doctor's Remarks……………………………………………………….…………

Doctor's Advice………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………….

Doctor's Name…………………………………………………………………..

Signature…………………………………………Rubber stamp ……………………

Date……………………

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA**

**SHULE YA SEKONDARI KITANDI**

**FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI NA TAARIFA ZA MZAZI NA MWANAFUNZI.**

**SEHEMU A: TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili (kama kwenye mtihani wa kumaliza elimu ya msingi)
   ……………………………………….……………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………………………….
3. Kabila …………………………………………………………………………………….
4. Mahali na Wilaya alipozaliwa ………………………………………………………..…….
5. Shule alipomaliza Darasa la Saba ……………… ……………………………………
6. Kidato anachokuja kuingia ……………………………………………………………….
7. Dini……………………………………………..
8. Michezo anayopendelea

| | |
|---|---|
| 1 | |
| 2 | |
| 3 | |

**UONGOZI WA SHULE**

Kazi yoyote ya uongozi aliyowahi kufanya kama vile. Kiranja, Kiongozi wa Kwaya, Ngoma Michezo n.k.

| S/N | NAFASI YA UONGOZI | SHULE | MWAKA |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |

Nathibitisha kwamba habari zilizotolewa hapo juu ni kamili na za ukweli

**Tarehe ……………………………** **saini…………………………………………**

**SEHEMU B: TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

i. Jina kamili.........................................................................................

ii. Kazi................................................................................................

iii. Makazi...........................................................................................

iv. Kata.....................................................................................................................

v. Tarafa..................................................................................................................

vi. Anwani ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………………………

vii. Namba ya simu ……………………………………………………………………

viii. Dini ………………………………………………………………………………………

ix. Anuani kamili ya nyumbani ambako mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo……………………

Ninaahidi kushirikiana na Walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapakazi na mwenye bidii ya kusoma.

Mimi ………..………..………...Mzazi/Mlezi wa………………………. ….ninathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi

Tarehe ……………………………… saini……………………………………

**MKATABA WA MWANAFUNZI KUHUSU KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

Mimi ………………………………………………..nimeyasoma kwa makini maelezo haya ya kujiunga na shule. Kwa hiari yangu nakubaliana nayo.

Naahidi nitaheshimu sheria, kanuni na taratibu zote za shule na miongozo mbalimbali itakayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Aidha naahidi kuwa kwa vyovyote vile sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai nikiwa shuleni au nje ya shule.

Endapo nitavunja sheria, kanuni, taratibu za shule, kushiriki katika migomo, fujo na kutenda makosa ya jinai, basi nichukuliwe hatua stahiki kulingana na kosa nitakalokuwa nimefanya.

Saini ya Mwanafunzi.....................................................................

Saini ya Mzazi.........................................................................

KITANDI SECONDARY SCHOOL
HEAD OF SCHOOL
P.O. Box 36
RUANGWA . LINDI

Saini ya Mkuu wa shule :

Muhuri wa mkuu wa shule:

**ORODHA YA VITABU VINAVYOHITAJIKA**

## GEOGRAPHY PAPER 1

1. Principles of physical geography by – F.J Monkhouse
2. A comprehensive approach to physical geography for secondary – by D.T Msabila
3. Practical geography for Africa – By John M. Prichard
4. Landforms in Africa – an introduction to geomorphology by colin buckle

## GEOGRAPH PAPER 2

1. Human and economic geography – by Goh cheng & Morgan
2. Advanced level geography course book – by Tanzania institute of education (TIE)
3. An integrated focal regional studies on human and economic geography advanced level paper II by D.T Msabila

## ENGLISH LANGUAGE 1

1. English for advanced secondary schools student's book form five- by TIE

## ENGLISH LANGUAGE 2

**a. NOVELS AND SHORT STORIES**

(i) Chinua Achebe – A man of the people ii. Ayi Kwei armah – The beautiful one are not yet born iii. Sago – His excellency the head of states

## b. PLAYS

(i) I will marry when I want – by Ngugi wa Thiong' o & Ngugi mirii
(ii) An enemy of the people – by H. Ibsen
(iii) The Caucasian – by B. Bretch
(iv) Betrayal in the City – by F. Imbuga

## c. POETRY

i. Selected poems – by Tanzania institute of education
ii. Poems from East Africa – by david cook et all N.B Make sure you come with TWO Titles from each part This list of English language is meant for HGL/HKL students

## HISTORY

(i) Rodney W. How Europe under developed Africa; Nairobi heineman Kenya (1992)
(ii) Nyeirenda H.D African in world history – a level certificates notes DSM (DUP)
(iii) D.W. Essay on the theory of imperialism DSM, THP(1979)
(iv) Lenin V.I (1992). Impelialism, the highest stage of capitalism Moscow progress
(v) N. Advanced level history notes selected topics for paper 1 & 2 (2002)

## KISWAHILI 1 & 2

(i) Kiswahili kidato cha tano – Taasisi ya Elimu
(ii) Kiswahili kidato cha sita – Taasisi ya Elimu
(iii) Vitabu vya Mashairi ,Tamthiliya na Riwaya kidato cha tano na sita